TANGAZO LA SERIKALI NA. 700 la tarehe 02 /12/2022

SHERIA YA MIPANGOMIJI,

(SURA YA 355)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 8(1))*

AMRI YA KUPANGA ENEO LA MWESE YA MWAKA, 2022

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Kupanga Eneo la Mwese ya Mwaka, 2022.

Kutangazwa kwa eneo la upangaji Sura ya 355

2. Eneo lililoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa eneo la upangaji kwa madhumuni ya Sheria ya Mipangomiji.

Mpango wa jumla na kina wa eneo

3. Mpango wa jumla na wa kina wa eneo lililoainishwa katika Jedwali unaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipangomiji na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Tanganyika.

## JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

Eneo la Upangaji lipo ndani ya mipaka ifuatayo:

“Unaanzia kwenye alama ya mpaka wa upimaji namba WDG 17 yenye majira - nukta 219392.33E, 9302784.88N; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini – Magharibi katika uelekeo wa N45°02'26"W kwa umbali wa kilomita 9.3 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba WDG 18 yenye majira - nukta 213133.73E, 9309037.30N; baada ya hapo unaelekea Kaskazini – Magharibi kwa kufuata mto Lwega hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba P1 yenye majira - nukta 202838.89E, 9312657.21N; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini – Magharibi katika uelekeo wa S71°03'53"W kwa umbali wa kilomita 5.7 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba VR 106 yenye majira - nukta 197402E, 9310792N; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini – Magharibi katika uelekeo wa N19°45'08"W kwa umbali wa kilomita 9.2 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba RV 46 yenye majira - nukta 194269E, 9319517N; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini – Magharibi katika uelekeo wa S07°57'00"W kwa

umbali wa kilomita 3.8 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba RV 14 yenye majira - nukta 194804E, 9323348N; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini – Mashariki hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba P2 yenye majira - nukta 200125.95E, 9323767.82N; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini – Mashariki katika uelekeo wa S59°44'54"E kwa umbali wa kilomita 5.4 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba P3 yenye majira - nukta 205503.80E, 9323485.20N iliyopo karibu na mto Mgungasi; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini – Mashariki kufuata mto msengusi hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba P4 yenye majira - nukta 237621.45E, 9277889.92N na alama ya mpaka ya upimaji namba 5 yenye majira - nukta 217548.57E, 9316698.79N; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini – Mashariki katika uelekeo wa S35°10'43" kwa umbali wa kilomita 7.3 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji iliyopo barabara ya Mpanda – Mwese (mlima Kasilipu) yenye majira - nukta 221825.51E, 9310767.65N; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini – Mashariki kufuata barabara ya Mpanda – Mwese hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba P6 yenye majira - nukta 223420.72E, 9310090.53N; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini – Magharibi katika uelekeo wa S27°14'55"W kwa umbali wa kilomita 8.5 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba WDG 17 mpaka ulipoanzia".

Dodoma,
8 Novemba, 2022

ANGELINE S. MABULA
*Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi*